**Learning by Ear 2009**

**Media & Information**

**Author: Hope Azeda**

**Redaktion: Ludger Schadomsky**

**Kisuaheli Translation:Eric Ponda**

**EPISODE 8**

| *CHARACTERS* | |
|---|---|
| Announcer: Male/female | |
| "Young Junior" | Male, 15 years old |
| "Sister P." | Female, 16 years old |
| "Charlie" | Male, 18 years old |
| "Ezra": | Male, 22 years old. Brother to "Young Junior". |
| Politician MP | Male, 50 years old+ |

**INTRO**

Hujambo msikilizaji wa Deutche Welle mahali popote ulipo na karibu kwa makala yetu ya 8 ya mfululizo wa vipindi vyetu vya Learning By Ear bado tukiwa tunazungumzia sekta ya habari na vyombo vya habari.Katika kipindi kilichotangulia Sister P, Young J na Charlie wanakutana na afisa wa baraza linalosimamia shughuli za vyombo vya habari, na kufahamu jinsi baraza hilo linavyosimamia maadili ya

uandishi na vyombo vya habari. Pia afisa huyo anawafahamisha kwamba baraza hilo linakabiliwa na hali ngumu ya kifedha na haliwezi kufadhili mradi wao wa kuanzisha kituo cha redio.Lakini kwa kuwa wameyavulia nguo, wanahabari hawa chipukizi hawaja kata tamaa na wanamiadi na mbunge Bw Christopher. Mbunge huyo anafurahia wazo la kuanzisha kituo cha redio, na ni kutokana na msisimko ambapo amewaalika wanahabari hawa ofisini mwake.

**SCENE ONE**

**Youth centre, morning. The place is busy with young people playing different games in the distance.**
**SFX Doors opening and closing and footsteps on a cemented floor.**

1. **Sister P:** Sasa tufanye nini, Young J,…. Charlie, au tusahau suala la kukutana na Mbunge huyu?

2. **Young J**: Tumsubiri kwa muda wa dakika nyingine 20 hivi.

3. **Sister P:** Kumbuka huyu ni mtu muhimu sana. Wajua ni mwanasiasa,na zaidi ni mbunge!.Tunabahati kwamba amekubali kukutana nasi. Ni fursa nzuri ambayo hatuwezi kuipoteza .

4. **Young J:** Hilo ndilo tatizo na Charlie . Yeye hataki kununua simu na sasa anatutatiza na mipango yetu kwasabbu hatuwezi kuwasiliana naye.

5. **Sister P:** Labda tuwapigie simu majirani kama wanaweza kumpitishia ujumbe?

**6. Young J:** Namfahamu vizuri sana Charlie, ni mtu wa kujigamba na nahakika hakuna mtu atakayeweza kumpitishia ujumbe huu.

**7. Sister P:** Sawa basi tusahau mambo ya Charlie, twendeni moja kwa moja hadi ofisi ya Mbunge!.

**8. Young J:** Tayari tumechelewa. Labda tukodishe Pikipiki.

**Sister P:** Pikipiki itanichafulia nywele zangu! .Unajua tunakutana na Mtu mashuhuri sana, na ni lazima tuonyshe kwamba sisi ni watu wa heshima na wenye nidhamu.

**10. Young J:** Kama ni hivyo basi itanibidi nibadilishe hii Jeans yangu uliohanuka .Utanitangulia ofisini..?

**11. Sister P:** Hapana ! Siwezi kuingia Ofisi ya mwanamume peke yangu!. Twende tu hivyo ulivyo…! kwanza Charlie huyu hapa amewasili

**Kommentar [TD1]:** As Charlie miraculously appears in the next scene I had him arriving in this.

**END SCENE**

**SCENE TWO**

**SFX At the MP's office. The atmosphere is calm, with light music playing in the background.**

**12. Sister P:** Habari Mheshimiwa? ,Tunakushukuru kwa mwaliko wako!.Mimi naitwa Sister P.

**13. Young J:** Naitwa Young J.

**14. Charlie:** Na mimi naitwa Charlie.

**15. MP:** Majina mazuri ya ujana hayo!. Nadhani sina haja ya kujitambulisha?

**16. Young J:** Si lazima Mheshimiwa, sisi sote katika jamii hii tunakufahamu vizuri.

**17. MP:** Sawa kabisa!. Je mungependelea kinywaji chochote? Soda au kahawa hivi.?

**18. Sister P:** Kinywaji ***chote*** Mheshimiwa!.

**19. MP:** Bora usema kinywaji ***chochote,*** maana ukisema kinuywaji ***chote*** hujafanya chaguo.

**20. Charlie**: Tutakunywa soda basi mheshimiwa!.

**SFX pressing phone buttons.**

**21. MP:** Sawa …! Hallo, naam unaweza kulitea soda tatu tafadhali. ..Asante!.

**22. Young J:** Mheshimia Ofisi yako ni nzuri sana

**23. MP:** Asanteni sana. Nilipata fursa ya kupitia mapendekezo muliyoandika kuhusu mradi wa kuanzisha kituo cha redio ya jamii, na nikafurahishwa sana na wazo hilo. Nani mubunifu wa wazo hili?

**24. Sister P:** Sisi sote watatu mheshimiwa! .

**25. MP:** Ni vizuri sana. Sirahisi kupata kundi la vijana wa rika lenu wakiwa na mawazo kama yenu… kuanzisha mradi wa maana wa aina hii.

**26. Young J:** Asante sana bosi .

**27. MP:** Mimi ni mheshimiwa.

**28. Young J:** Asante sana Mheshimiwa.

**29. MP:** Kituo cha redio kinachosimamiwa na vijana ni mradi wa maana sana unaoweza kuwaepushia vishawishi vya kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya na ulevi wa kupindukia. Na klabu yenu inajulikana kama***… C.D.C?***

**30. Charlie:** Hapan ni ***D.C.C***. Yaani Dot.Com.Club na kituo cha redio kitajulikana kama ***Dot.Com FM stereo.***

**SFX Knock on the door, silence and door opens, bottles and glasses on the table and opening sodas**

**31. Sister P:** Asante.

**32. MP:** Mnazungumzia mradi wa kuanzisha kituo cha redio na hii ndio sababu iliyonifanya kuwaita hapa ofisini mwangu. Nafahamishwa kwamba tatizo lenu kubwa ni kupata fedha za kufadhili mradi huu. Je mumefanikiwa kulitatua tatizo hili?

**Kommentar [TD2]:** This whole Sir / Honourable thing I don't understand. In UK some MPs are "honourable" which means they are a kind of lawyer, but they would not be addressed Honourable apart from in the Houses of Parliament.

**33. Charlie**: Bado mheshimiwa!.Tumeweza tu kukusanya nusu ya kiasi kinachohitajika ,lakini bado hatujafanikiwa kupata kiasi kilichoalia kufanikisha mrdi huu.

**34. MP:** Sawa mimi nitawasaidia kadri ya uwezo wangu.

**35. Sister P:** Tutashukuru sana boss !

**36. MP:** Mimi si bos ni Mheshimiwa ! Nitajaribu kusaidia. Jukumu letu sisi viongozi ni kuwasaidia vijana kama nyinyi kujiendeleza na kulijenga taifa letu.

**37. All:** Tunashukuru sana Mheshimiwa .

**38. Young J:** Pia tumewasilisha maombi yetu ya kupewa leseni ya kuanzisha kituo hicho lakini tunafahamihwa kua huenda itachukua muda mrefu iwapo hakuna mtu wa kutusaidia .

| **SFX: Knocks the tray and sodas go falling on the table.** |
| --- |

**39. Sister P:** (**Upset).** Young Junior, Sasa unafanya nini ?

**40. Young J**: Samahani, Boo…pole…, Mheshimiwa…Siku…..…

**41. MP**: Usijali. Tuna mambo muhimu zaidi ya kuzingatia kuliko hayo ya kumwagika kwa Soda. Sasa niambieni , mumesema huu ni mradi wenu sivyo.Hamuna meneja au msimamizi mwengine yoyote.?

**42. Charlie:** Hapana huu ni mradi wetu wenyewe. Sisi ndio meneja na tunasimamia kila kitu.

**43. MP:** (**Laughs)** Sawa.Je munafahamu kwamba uchaguzi utaandaliwa katika kipindi cha mwaka mmoja ujao?

**44. Sister P:** Ndio tunafahamu hilo.

**45. MP:** Vyema. Na munafahamu uwezo wa vyombo vya habari katika kuwashawishi wananchi wakati kama huu.?

**46. Young J**: Ndio . Chombo cha habari kinaweza kukujenga au kubomoa. Inategemea tu jinsi unavyokitumia.

**47. MP:** Sasa ninachotaka kuwaambia ni kwamba, nitajaribu kumsaidia lakini nanyi kwa upande wenu munisaidia kupitia stesheni hii ya Dot.Com FM kuelezea sera na maongozi ya chama changu.

**48. Sister P:** Samahani hatujakuele?

**49. Charlie:** Yaani unataka kumiliki kituo hiki?

**50. MP:** La hasha bado kitaendelea kuwa chini ya usimamizi wenu lakini wanasiasa kutoka vyama vingine hawataruhusiwa kukitumia au kushirikishwa katika vipindi vyenu na hata mahojiano.

**51. Young J**: Mheshimiwa sisi bado wanafunzi katika chuo cha mafunzo ya uandishi wa habari.Na kimsingi ni

kwamba kama waandishi wa habari hatupasi kuegemea upande wowote katika uandishi wa habari.

**ster P:** Ufupi ni kwamba hatuwezi kuenda kinyume na maadili ya uandishi.

**53. MP:** (**laughs)** Nyini bado vijana,kweli munahitaji kujifunza mengi ili kutofautisha suala la maadili na ukweli wa mambo!.

**54. Charlie:** Hiyo ni kumaanisha nini?

**55. MP:** Sawa.., labda niulize, kwanini mukaamua kuanzisha kituo cha redio?

**56. Sister P:** Kwa sababu tumechoshwa na vipindi vinavyopeperushwa na stesheni ya taifa.

**57. Charlie:** Na muziki wa zilizopendwa.

**58. Young J:** Ndio sababu tukaamua njia pekee ya kubadilisha hali hii na kuweza kucheza muziki wetu wenyewe ni kuanzisha kituo hiki. Mbali na hayo pia tunataka kuihudumia jamii.

**59. MP:** Na ndio sababu nataka kumrekebisha .Kila kitu mnacho sema ni kweli, lakini ni upuzi mtupu!. Mnaweza kusahau mambo ya burudani. Kwani kila

jambo mutakalofanya mutahitaji kula ,kusafiri na kuishi maisha mazuri. Nani akaye mgharamia mambo yote haya?.Fungueni macho na masikio vijana!

**60. Charlie**: Unasemaje, Sister P?

**61. Sister P**: Sidhani kama hiyo ndio sababu ya kutaka kuanzisha chombo cha habari.

**62. MP**: Mulitaja suala la leseni .Kwani inachukue muda mrefu hivyo?. Nambieni kama mnataka msaada wangu nami nitahakikisha munapata leseni hiyo katika muda wa siku moja tu? Yote haya hutegemea jinsi unavytumia ofisi yako. Wakati wa kampeini nataka mzungumzie yote mazuri yaliyotekelezwa na chama changu na kisha itamulipa!.

**63. Young J:** Ni suala gumu sana..!

**64. MP:** Hakuna ugumu wowote hapa.. hee ugumu uko wapi? Nampa muda wa kufikiria kisha munipe jibu.

**SCENE THREE**

**65. Ezra's bedroom. Night.**

**SFX slow music playing and switching off the light.**

**66. Young J**: Usiku mwema, Ezra.

**67. Ezra:** Usiniambie tayari unaenda kulala?

**68. Young J**: Sio eti naendea kulala, lakini nataka tu kutafakari yote kuhisiana na mradi huu wa kituo cha redio.

**69. Ezra:** Lakini hujaniambia yaliyotokea leo. Mambo yalikwenda vizuri?

**70. Young J**: Leo ilikuwa siku nzuri sana.

**71. Ezra:** Hebu funga huo Muziki…nataka kusikia yaliyotokea katika siku hii nzuri!

**FX: Bed creaking, music is switched off.**

**72. Ezra:** Ehe, niambia nini kilichotokea?

**73. Young J** Leo tulialikwa katika ofisi ya Mbunge Christopher's.
.

**74. Ezra:** Kweli? Vizuri sana ….ehhe hebu niambia!.

**75. Young J**. Usiwe na pupa, sijakwambia kilichotokea.

76. **Ezra:** Eendelea!.

77. **Young J**: Akatuahidi kutusadiai na kiasi cha fedha zilizosalia kukamilisha mradi wetu na msada mwengine wowote kufanikisha mradi huu.

78. **Ezra:** Kweli wache wee.? Kisha…..?

79. **Young J:** Aahh si unawajua wanasiasa wetu, kwa sharti moja tu…! kwamba pindi kituo kitakapoanzishwa aweze kukitumia kama chombo kuelezea sera na maongozi ya chama chake. Na ni wafuasi wa chama hicho pekee watakaoruhusiwa kushiriki kwenye vipindi na mahojiano mbali katika redio hiyo.Mbali na hayo tuandike habari za kukisifu chama hicho!.

80. **Ezra:** Na kwa kumjibu mkamwambiaje?

81. **Young J**: kwanza tulisita.. kisha tukashawishika!.

82. **Ezra:** Sawa lakini ushauri wangu ni kwamba, msahau kabisa msaada huo wa masharti. Maana utavuruga malengo yanu na mwito wa kuihudumia jamii.

83. **Young J:** Ezra!

**84**: **Ezra** Yaani mutakuwa vibaraka wa wanasiasa na kupoteza muelekeo wenu mbali na kuangukia

mtego wa ufisadi, kwasababu mutashawishiwa kutangaza habari za uongo. Ndugu zangu wapenzi , lazima mukatae vishawishi iwapo mnataka kutimiza ndoto yenu.

**END EPISODE**

**OUTRO**

Naam,bila shaka kama mulivyosikia,wanahabari hawa sasa wako katika njia pande kukubali msaada wa masharti au kudumisha maadili ya taaluma yao. Kwa ufupi lengo kubwa la mwanasiasa huyu ni kuwahonga wanahabari ili kutumia kituo hicho kama jukwaa na chombo cha kampeini wakati wa uchaguzi mkuu.Je umewahi kushuhudia ushawishi wa aina hii kutoka kwa wanasiasa nchini mwako. Je wewe ni miongoni mwa wanahabari wanaokubali hongo kutoka kwa wanasiasa ili kupinda maadili mema na kuandika tu habari za kuwasifu.Tutumie maoni yako kupitia mtandao wetu wa dw-world.de/lbe nasi hapa Bonn tutafurahi kupokea maoni hayo. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.